TANGAZO LA SERIKALI Na. 863 la tarehe. 18/10/2024

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA MIJI),
(SURA YA 288)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 89)*

## SHERIA NDOGO YA MAREKEBISHO YA SHERIA NDOGO YA KILIMO NA USALAMA WA CHAKULA YA HALMASHAURI YA MANISPAA YA MTWARA-MIKINDANI YA MWAKA 2024

Jina

TS. Na. 219 la 2024

**1**. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Marekebisho ya Sheria Ndogo ya Kilimo na Usalama wa Chakula ya Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara-Mikindani ya Mwaka 2024, na itasomwa pamoja na Sheria Ndogo ya Kilimo na Usalama wa Chakula ya Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara-Mikindani ya Mwaka 2024, ambayo katika Sheria Ndogo hii inarejewa kama "Sheria Ndogo kuu".

Marekebisho ya kanuni ya 3

**2**. Sheria Ndogo kuu inarekebishwa katika kanuni ya 3 kwa kuongeza tafsiri mpya ifuatayo kwa kuzingatia mtiririko wa kialfabeti:

"mkuu wa soko" maana yake ni mtumishi wa umma aliyeteuliwa na Halmashauri kusimamia shughuli zote katika soko linalomilikiwa na Halmashauri;".

Marekebisho ya kanuni ya 5

**3**. Sheria Ndogo kuu inarekebishwa kwa kufuta na kuandika upya kanuni ya 5 kama ifuatavyo:

"Wajibu wa Serikali ya Mtaa

**5**. Serikali ya mtaa itakua na wajibu wa-

(a) kutenga ardhi kwa ajili ya kilimo na malisho ya mifugo, maeneo ya ufugaji wa nyuki na mabwawa ya kufugia samaki;

(b) kuhakikisha kwamba kila mkazi anapata ardhi ya kutosha kwa ajili ya kutekeleza kauli mbiu ya kilimo kwanza kwa kushirikiana na uongozi wa kitongoji;

(c) kutoa elimu kwa wananchi kuhusu uhifadhi wa chakula ikiwemo kununua chakula cha kutosha kabla ya bei kupanda;

(d) kuhakikisha kwamba mkulima anamuuzia mazao mnunuzi mwenye kibali cha Halmashauri na leseni ya kununua mazao;

(e) kusajili wakulima na mazao wanayolima;

(f) kuhakikisha kuwa sheria zinazosimamia mazao na kanuni zake zinatekelezwa; na

(g) kuhakikisha kuwa masoko rasmi ya kuuza mazao ya wakulima yanaanzishwa.”.

Kufutwa kwa kanuni ya 11

**4.** Sheria Ndogo kuu inarekebishwa kwa kufuta kanuni ya 11.

Marekebisho ya kanuni ya 12

**5.** Sheria Ndogo kuu inarekebishwa katika kanuni ya 12, kwa-.

(a) kufuta maelezo ya pembeni na badala yake kuweka maelezo yafuatayo:

“Ukaguzi”;

(b) kuongeza maneno “ndani ya muda wa saa za kazi” mara baada ya neno “yoyote” lililopo katika aya (b); na

(c) kufuta alama ya nukta mkato iliyopo mwishoni mwa aya (e) na badala yake kuweka alama ya mkato.

Marekebisho ya kanuni ya 15

**6**. Sheria Ndogo kuu inarekebishwa katika kanuni ya 15, kwa-

(a) kufuta kanuni ndogo ya (3) na kuiandika upya kama ifuatavyo:

"(3) Endapo mfugo utakutwa unazurura ovyo mtaani au kwenye sehemu ambazo hazijaruhusiwa kwa ajili ya malisho, mfugo huo utakamatwa na Halmashauri na mwenye mfugo atawajibika kulipa faini iliyoainishwa katika Jedwali la Kwanza."; na

(b) kuongeza mara baada ya kanuni ndogo ya (3) kanuni ndogo zifuatazo:

"(4) Ndani ya kipindi cha siku saba tangu kukamatwa kwa mfugo na baada ya kupata idhini ya Mahakama, Halmashauri itakuwa na haki ya kuuza kwa mnada mfugo uliokamatwa na fedha zitakazopatikana zitarejeshwa kwa mmliki wa mfugo huo baada ya kutoa faini inayodaiwa, gharama za kuhifadhi mfugo, gharama ya Mahakama na gharama ya mnada.

(5) Ndani ya muda usiopungua siku tatu kabla ya kuuza mfugo kwa mnada, Halmashauri itamjulisha mmliki na umma kuhusu kusudio la kuuza mfugo huo kwa mnada.

(6) Endapo itatokea kifo cha mfugo kutokana na sababu yoyote, Halmashauri haitawajibika na ulipaji wa gharama zozote isipokuwa kama kifo hicho kitakuwa kimesababishwa kwa uzembe wa Halmashauri.".

Dodoma,
29 Agosti, 2024

MOHAMED OMARY MCHENGERWA,
*Waziri wa Nchi -OR-Tamisemi*